ZURA

Zanzibar Utilities Regulatory Authority

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR**

08/05/2025

**TAARIFA KWA UMMA JUU YA BEI ZA MAFUTA KWA MWEZI MEI 2025**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inatangaza Bei za Mafuta kwa Mwezi Mei 2025 zitakazoanza kutumika rasmi kuanzia Siku ya **Ijumaa, Tarehe 09/05/2025**.

Mamlaka hupanga bei kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za Mafuta Duniani (Platts Quotations).
- Gharama za uingizaji Mafuta katika bandari ya Tanga.
- Gharama za Mabadiliko ya Fedha za kigeni zinazotumika kununulia mafuta.
- Gharama za Usafiri, Bima na 'Premium' hadi Zanzibar.
- Kodi na Tozo za Serikali.
- Kiwango cha faida kwa Wauzaji wa Jumla na Reja Reja.

Bei za mafuta kwa Mwezi Mei, 2025 ni kama zifuatazo:

| AINA YA MAFUTA | BEI YA MWEZI APRIL, 2025 (TZS/LITA) | BEI YA MWEZI MEI, 2025 (TZS/LITA) | TOFAUTI (TZS/LITA) | TOFAUTI ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| PETROLI | 2,949 | 2,969 | 20 | 0.68 |
| DIZELI | 3,194 | 3,191 | -3 | -0.09 |
| MAFUTA YA TAA | 3,200 | 3,200 | 0 | 0 |
| MAFUTA YA NDEGE | 2,537 | 2,537 | 0 | 0 |

Sababu za mabadiliko ya Bei za Mafuta kwa Mwezi Mei, 2025 yametokana na mabadiliko ya gharama za uingizaji wa mafuta na mabadiliko ya wastani wa thamani ya Fedha ya kigeni ukilinganisha na Shilingi ya Tanzania.

Aidha, Mamlaka inawahimiza Wananchi kununua Mafuta katika Vituo halali vya Mafuta na kudai Risiti za Kielektroniki kila wanaponunua Mafuta.

MAMLAKA YA UDHIBITI HUDUMA ZA MAJI & NISHATI ZURA Zanzibar Utilities Regulatory Authority P.O.Box 2238 ZANZIBAR

**IMETOLEWA NA KITENGO CHA UHUSIANO (ZURA)**

+255 24 294 1190
S.L.P 2238

info@zura.go.tz
zura.go.tz

Makao Makuu ZURA
25 Barabara ya Julius Nyerere
70473 Mjini Magharibi, Maisara, Zanzibar